advansmart

Advansmart Business Consultants
Certified Public Accountants in Public Practice
Old Dar Es Salaam Road, 2nd Floor NHC Building
P.O. Box 2364 Morogoro | Tel: + 255 655 303091
Email: info@advansmart.co.tz |Website: www.advansmart.co.tz

**Kumb: ADV/GC/2025/03** **Tarehe: 1st Agosti 2025**

________________________________
________________________________
________________________________
________________________________

**YAH: MWALIKO WA KUHUDHURIA SEMINA YA UHASIBU NA MABADILIKO MAPYA YA SHERIA NA KANUNI ZA KODI ITAKAYOFANYIKA MOROGORO, TAREHE 28 – 29 AGOSTI 2025.**

Tafadhali, husika na mada tajwa hapo juu.

Tunayo furaha kukuarika kwenye semina/mafunzo maalum ya Uhasibu na Mabadiliko ya Sheria za Kodi yatakayofanyika katika ukumbi wa mafunzo na mikutano uliopo katika Ofisi za Advansmart, Jengo la NHC ghorofa ya pili, Ofisi namba 205 na 206, Morogoro Mjini. Semina hii ni muhimu sana kutokana na mabadiliko kadhaa kanuni za uhasibu (IFRS na IPSAS) zilizoanza kutumika tarehe 1 Januari 2025 na zitakazo anza kutumika tarehe 1 Januari 2026 pia kuna mabadiliko kadhaa ya sheria na kanuni za kodi yaliyofanyika katika sheria ya fedha ya mwaka 2025 ambayo yamepelekea mabadiliko ya sheria mbalimbali za kodi. Mabadiliko hayo ya sheria na kanuni yameanza kutumika tarehe 1 Julai 2025. **Semina/Mafunzo yatakuwa ya siku mbili tarehe 28 na 29 Agosti 2025.**

**Lengo la Mafunzo**

- Kuwapa washiriki uelewa wa kina wa maeneo muhimu ya kuzingatia katika mabadiliko ya sheria ili kuepuka au kupunguza hatari ya kutozingatia sheria za kodi (kupunguza faini na adhabu ambazo zinapunguza fedha za kuendesha taasisi, shirika ua kampuni).
- Kuwapa washiriki uelewa wa kina wa kanuni mpya za uhasibu (IFRS & IPSAS) ili kuboresha utayarishaji wa hesabu za fedha ambao unazingatia uwazi na misingi ya uhasibu, sheria na kanuni.
- Kuwapa washiriki maarifa juu ya mbinu bora za utunzaji wa kumbukumbu za kodi na uhasibu, na jinsi ya kujiandaa na kukabiliana na ukaguzi wa kodi.

**Mada zitakazowasilishwa na kujadiliwa**

- Mabadiliko mapya ya Sheria za Kodi, na matokeo yake katika utekelezaji wake.
- Ukokotoaji wa kodi (CIT, PIT, WHT, PAYE, SDL, VAT, Stamp duty, etc), uwasilishaji wa ritani za kodi na ulipaji wa kodi wa hiari.
- Utunzaji sahihi wa kumbukumbu za kodi na uhasibu,
- Mbinu za kujiandaa na kukabiliana na ukaguzi wa kodi.
- Mabadiliko mapya ya viwango vya kimataifa vya uhasibu (IFRS & IPSAS)
- Mwongozo mpya wa uhakiki wa Hesabu za fedha kwa taasisi, makampuni na mashirika uliotolewa na NBAA ulioanza kutumika tarehe 1 Julai 2025

**Ada ya Ushiriki, Usajili na Malipo**

Ada ya Kushiriki ni TZS 300,000.00 kwa kila mshiriki, kwa ajili ya chai, chakula na vinywaji na nyenzo za mada zitakazowasilishwa, aidha vyeti vitatolewa vya saa 16 za CPD ambazo zinatambuliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).

Tafadhali thibitisha kuhudhuria kwako kwa kufanya malipo kabla ya tarehe 27 Agosti 2025 kupitia Akaunti ya Benki ya NMB 24910003488 Jina la Akaunti: Advansmart Business Consultants.

**Mawasiliano**

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na Bw. Deogratius Lyimo +255 617 667 791 au Bi. Mwajuma Uwesu +255 683 986 436.

Wako,

Ezekiel Emmanuel
Mkurugenzi